# Learning by Ear 2010 – "Against the Current" – Urban Exodus

## Episode 04: "Every woman's dream"

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

CHARACTERS:

Onyesho la 1:

- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- **HADIA** (UMRI MIAKA 45, MAMA YAKE NANA)

Onyesho la 2:

- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- **NANA** (UMRI MIAKA 22, MWENYEKITI WA CHAMA CHA VIJANA))

Onyesho la 3:

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI WA MIAKA 57)
- **BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI MIAKA 24,MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)

**<u>Intro :</u>**

Karibu kwenye *Learning by Ear*. Kipindi cha leo ni cha nne cha mfululizo wetu kuhusu uhamiaji mjini unaoitwa: “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko”.

Tunafuatilizia masaibu ya Ben, Baki na Zeina-vijana watatu wasio na ajira walio na shahada za chuokikuu waliohama mjini na wanaotaka kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini.

Katika kipindi hiki cha nne, hatua ya vijana hawa kurejea kijijini inasababisha hisia zisizotarajiwa miongoni mwa wanakijiji. Je vijana hawa wataweza kuwavutia wanakijiji? Tega sikio kwa makini, upate kufahamu!

**Scene 1: A village road.**

**ZEINA, HADIA.**

1. **ATMO: POUNDING, CONVERSATION AND TRAVELLING SALESMEN SHOUTING, MOOING IN THE DISTANCE, CARS**

2. **ZEINA** Shangazi Hadia! Habari gani?

3. **HADIA** Kama wataka kujua, njoo nyumbani. Unakumbuka njia ya kuja nyumbani? Natumai ulikamilisha masomo yako.

4. **ZEINA** Naam, Nilimaliza. Sasa yapata miaka mitatu. Lakini hakuna ajira.

| | | |
|---|---|---|
| **5.** | **HADIA** | Usife moyo! Kwa ujuzi na ukakamavu wako, bila shaka utapata kazi. Na vipi ndoa? Umeliwazia hilo? |
| **6.** | **ZEINA** | Ndiyo, bila shaka! |
| **7.** | **HADIA** | Tahadhari, wakati unayoyoma. Kila jambo na wakati wake …. Hivi ndivyo ninavyomwambia binamu yako Nana kila wakati. |
| **8.** | **ZEINA** | Nana yuko hapa? Hajambo? |
| **9.** | **HADIA** | Amekuwepo hapa kwa muda wa mwaka mmoja. Sijui anataka nini huku. Hawezi kumpata mume na kuzaa watoto huku. Hapa kuna wanaume vizee pamoja na wahuni ambao hata kujilisha wenyewe hawawezi. |
| **10.** | **ZEINA** | Si kwamba mjini ni bora. Ukosefu wa ajira na dhiki, sawa na hapa. Je, Nana anafanya kazi? |
| **11.** | **HADIA** | Kila mara yuko kwenye ofisi ya chama cha vijana lakini hiyo si kazi. Ni kazi ya kujitolea. Yeye ndiye mwenyekiti. Kila wakuu wanapopitia kijijini, utamwona Nana hapo. Ninatumai siku moja atabahatika kupata mume… |
| **12.** | **ZEINA** | Lakini pengine hajalitilia hilo maanani. |
| **13.** | **HADIA** | Huo ndio wasiwasi wangu. Mwezi uliopita aliikataa posa nyingine. Unajua nani? Tingo, yule mfanyibiashara. Mwanamume anayeweza kufanya jambo lolote kijijini hapa. Ni tajiri na ana ushawishi mkubwa na hana mke. |

| | | |
|---|---|---|
| **14.** | **ZEINA** | (**a bit absent-mindedly**) Unajua, shangazi, sijui kwa nini hatujitambui vinginevyo ila tu kama wake za watu... |
| **15.** | **HADIA** | (**hesitatingly**) Hmm…. Eeeh… Nifanyie hisani moja. |
| **16.** | **ZEINA** | Bila shaka, shangazi. |
| **17.** | **HADIA** | Nenda kamuone. Tafadhali msihi aandamane nawe kurudi mjini. Mjini kuna nafasi nyingi. Utanifanyia hisani hiyo? |
| **18.** | **ZEINA** | Aah… Hilo jambo gumu kidogo kwangu… Nimerejea kabisa hapa kijijini kwa kuwa mambo hayaendi sawa mjini. |
| **19.** | **HADIA** | Hali ni ngumu kila mahali. Ninajua hilo. Lakini hapa mambo ni mabaya zaidi. Rudi mjini pamoja na mwenzio huyo. Shika hizi hapa! |
| **20.** | **ZEINA** | Nini? |
| **21.** | **HADIA** | Fedha kidogo. Ni nauli yenu – nyote wawili. Pokea hizi fedha kisha uende ukaseme naye! Zipokee! |
| **22.** | **ZEINA** | Shangazi Hadia…. (**sighing**), sijui nikuelekeze vipi unifahamu! Nimechoka kuzunguka barabarani mjini. Sasa ninataka kuishi na kufanya kazi hapa. |
| **23.** | **HADIA** | Kijijini hapa? |
| **24.** | **ZEINA** | Ndiko nyumbani kwetu. Au siyo? |
| **25.** | **HADIA** | (**clicking her tongue**) Ama kweli!... Chuo kikuu kinakupa ujuzi lakini kinakupokonya akili. Hakuna la maana linalotendeka hapa. Hakuna awezaye kuishi hapa… |

**26. ZEINA** Ndiyo sababu…

**27. HADIA** (**angrily**) Upuzi mtupu! Kusema kweli!

**28. SFX: STEPS GOING AWAY FAST**

**29. ZEINA** Shangazi Hadia!... Subiri! Ngoja nikueleze. Shangazi!

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: Nana's office.**

**NANA AND BAKI**

**30. ATMO: SOUNDS OF OFFICE**

**31. SFX: KNOCK AT THE DOOR**

**32. NANA** Karibu!

**33. SFX: DOOR OPENS AND CLOSES AGAIN**

**34. BAKI** Nana hujambo? Habari gani?

**35. NANA** (**Reserved**) Alaa! Kumbe ni wewe, Baki. Nilidhani utarudi mjini bila kunipitia kunijulia hali.

**36. BAKI** Nisingefika huko mjini lau ningeondoka bila kukupitia

unilekeze njia!

37. **NANA** Nani kama mimi?

38. **BAKI** Una nguvu za ajabu, Nana! Hakuna litendwalo humu kijijini pasi nawe kuliidhinisha. Naomba kuketi.

39. **NANA** Karibu ukae.

40. **SFX : NOISE OF A CHAIR BEING MOVED**

41. **NANA** Je, hizi habari za chama cha ushirika ni kweli?

42. **BAKI** Kweli kabisa!

43. **NANA** Ebu nielezee kinagaubaga kuhusu habari hizo.

44. **BAKI** Nana, ninajua una habari zote.

45. **NANA** Kuna uvumi mwingi hapa kijijini. Bora nipate habari za uhakika.

46. **BAKI** Tutakuja kukupa habari rasmi wakati ufaao. Usijali.

47. **NANA** (**offended**) Ahaa, kumbe? Mtakapomaliza kuwaambia watu wote muhimu?

48. **BAKI** Usiwe hivyo nawe!

49. **NANA** Niwe vipi?

50. **BAKI** Tutakufahamisha kuhusu mradi wenyewe na kukuomba

ushiriki.

**51.** **NANA** Nitakwambia ukweli. Mmesababisha hali ya suitafahamu hapa kijijini kwa dhana zote hizo na uvumi usiokuwa na msingi. Kwanini msiwaite wanakijiji wote uwanjani na muwafahamishe kuhusu mradi wenu?

**52.** **BAKI** Tulidhamiria kwanza kuzungumza na watu ana kwa ana kabla ya kupanga mkutano wa hadhara.

**53.** **NANA** Sawa, mkimaliza kuwafahamisha watu wenye ushawishi mkubwa kuhusu mradi wenu, natumai mtanikumbuka !

**54.** **BAKI** Bila shaka! Nimeshakwambia kwamba tutatenda hilo… Tunaanzisha chama cha ushirika wa ukulima kuratibu ujuzi walio nao wakazi wa kijijini. Tungependa kuanzisha nafasi za ajira, kuongeza mavuno na pia kuimarisha mapato ya wanakijiji. Aidha tungependa kuhakikisha tumekabiliana na upungufu wa chakula.

**55.** **NANA** Kwani mnafikiri ninyi ni nani? Serikali?

**56.** **BAKI** Hapana.

**57.** **NANA** Chama chetu cha vijana hakiungi mkono upande wowote wa siasa.

**58.** **BAKI** Kundi letu si chama cha kisiasa. Hatuna ushirika na makundi yoyote yenye ushawishi mkubwa.

**59.** **NANA** Hmmm!

**60. BAKI** Ni fikra ya Ben. Yeye ndiye aliyetuhusisha mimi na Zeina. Lakini tunahitaji watu wengi ili mradi huu ufanikiwe. Watu wazuri… kama wewe.

**61. NANA** Umeshakuwa mtu wa kutaniana?

**62. BAKI** Nana nisikize. Wewe ndiye mwenyekiti wa chama cha vijana wa hapa kijijini. Unaweza kufikisha habari hii kwa kundi kubwa zaidi. Ikiwa utajiunga nasi, vijana wote watashirikiana nasi.

**63. NANA** Na mtanipa wadhifa gani?

**64. BAKI** Hatutafuti wafanyikazi sisi. Tunawataka watu watakaojishughulisha na chama cha ushirika, ambacho kitaimarisha mapato na kutoa ajira kwa kila mtu. Tumepania kubadilisha maisha ya hapa kijijini. Kwa kila hali.

**65. NANA** Aha, mabadiliko kweli hayo!

**66. BAKI** Tungependa wakazi wa kijiji hiki wajitosheleze kwa chakula. Tungependa kuwaondolea vijana tatizo la ukosefu wa kazi na maisha yao ya ukimbizi. Tunataka kila mtu apate hadhi na afurahie kuweko kijijini hapa. Hatutaraji kupawa msaada na YEYOTE.

**67. NANA** Unayosema yanavutia. Lakini hapa vijana wasipokimbilia mjini, huishia kuwa watumizi wa dawa za kulevya au kuwa watumwa wa Tingo huyo tumjuao jinsi alivyo na ushawishi. Chama chetu kina nia ya kubadilisha mwelekeo na kukabiliana vikali na huyo Tingo. Hata hivyo si jambo rahisi!

**68.** **BAKI** Lakini si kwamba haiwezekani?

**69.** **NANA** Sijui… Vigumu sana kubadilisha akili za watu, ni vigumu sana kubadilisha mitazamo ya watu wa hapa. Watu wanavyoishi hapa utadhani hawana la kutenda kubadili hali zao, kama kwamba hali haiwezi kubadilika.

**70.** **BAKI** Na chama chako kinafanya nini kukabiliana na hali hii?

**71.** **NANA** Mikutano ya kuwahamasisha na kuwapa taarifa. Lakini kila mara watu huuliza swali lile lile moja: TUFANYE NINI? Na mimi sina jawabu kwa sababu sina uwezo wa kulikabili na kwa hivyo mimi hujinyamazia…

**72.** **BAKI** Tutapendekeza mbinu nyingine na tujaribu kutafuta njia ya kutekeleza.

**73.** **NANA** Wazo zuri hilo!

**74.** **SFX: NOISE OF A CHAIR AS SOMEBODY GETS UP - STEPS MOVING AWAY SLOWLY**

**75.** **BAKI** Mimi, Ben na Zeina tutakuja kuwasilisha mradi wetu kwako. Kirasmi na kwa kina.

**76.** **SFX: DOOR OPENS**

**77.** **NANA** Unijulishe mapema ili niwaeleze wanachama wetu wafike.

**78.** **BAKI** Sawa! Kwaheri Nana, tutaonana karibuni.

----- MUSIC -----

**Scene 3: At Ben's. Courtyard - calm.**

**KABO, BEN, ZEINA AND BAKI.**

**79. ATMO: CALM COURTYARD. CRICKETS, HENS, HAMMERING IN THE DISTANCE.**

**80. SFX: INSTRUMENTAL MUSIC, LOW VOLUME, FROM RADIO**

**81. KABO** Leo nimefanya kazi kweli! Tangu asubuhi nimekuwa nikizunguka na kuzungumzia hiki chama cha ushirika, nilizungumza na mkuu wa kijiji, nimekwenda msikitini na pia kanisani. Wakazi wengi hapa wenye ushawishi wanaunga mkono mpango huu.

**82. ZEINA** Sisi tumeshinda kutwa nzima tukimsubiri mkuu wa idara ya maendeleo ya mashambani.

**83. BEN** Tulimsubiri ofisini asubuhi wala hakuja.

**84. KABO** Amekuwa nasi hapa kwa muda wa miaka minane sasa!

**85. BAKI** Mbona hamfanyi bidii awaondokee?

**86. KABO** Maadamu mtumishi wa umma hatatizani na wanakijiji au wanasiasa, hakuna anayemjali hata kama haimudu kazi yake vizuri, awe ovyo au mla rushwa.

| | | |
|---|---|---|
| **87.** | **BAKI** | Nilikutana na Nana, mwenyekiti wa chama cha vijana. Ana shaka. Anadhani tunataka kuanzisha chama cha kisiasa... |
| **88.** | **ZEINA** | Mbona ukamtembelea Nana peke yako? |
| **89.** | **BAKI** | Nilikuwa napita tu karibu na afisi yake. Kisha nikaingia ndani kumjulia hali… Halafu... |
| **90.** | **ZEINA** | Tulikubaliana tuwe tukiandamana wawili wawili tunapokwenda kuzungumza na watu! |
| **91.** | **BAKI** | Naam tulikuwa tumekubaliana hivyo! Na ndivyo nilivyomwambia. Alisema tumjulishe mapema ili awajumuishe wanachama wa chama chake. |
| **92.** | **BEN** | Iwapo hilo litafanyika, itakuwa nafuu kwetu. |
| **93.** | **ZEINA** | Ndiyo, lakini sivyo tulivyokubaliana kwamba tungewatembelea viongozi wa hapa kijijini. |
| **94.** | **BAKI** | Samahani… Nili… |
| **95.** | **ZEINA** | Kuna haja gani ya kuamua mambo ya kutenda ikiwa kila mtu atajitendea atakavyo? |
| **96.** | **BAKI** | Sikutaka… Naomba msamaha... |
| **97.** | **ZEINA** | Hutasamehewa vivi hivi! |
| **98.** | **BEN** | Ebu yaache hayo Zeina! Ameomba msamaha. |
| **99.** | **KABO** | Wahenga walisema jambo la kutenda mtu anapofanya kosa ni moja - kumrekebisha. |

**100. BAKI** Ninajua linalomsumbua ni kwamba tulikuwa mimi na Nana peke yetu.

**101. ZEINA** Unasema nini?

**102. BAKI** (**excited**) Kwamba una wivu!

**103. ZEINA** Ati? Unadhani kuna msichana yeyote anayeweza kukuonea wivu wewe?

**104. BAKI** Zeina ...

**105. ZEINA** (**interrupting**) Wasichana bila shaka wanaokupenda wapo. Lakini je wewe? Unashughulika na nini? Una jingine unalofikiria ila nauli yako ya ndege na viza yako? Hudhani kwamba kuna msichana hapa anayetamani kumpata mwanamume anayeishi Marekani?

**106. BAKI** Ninakutania nawe…

**107. SFX: FURIOUS STEPS GOING AWAY**

**108. ZEINA** **(shouting from afar)** Bila shaka, umefanikiwa!

**109. BAKI** Zeina! Zeina! Subiri!

**110. SFX: STEPS RUNNING AWAY**

**111. BAKI** (**going away**) Zeina, hujanielewa… Nilitaka kuzijua hisia zako… Ninajua nililosema si sawa lakini …

**112. KABO** Hivi ndivyo walivyo?

**113. BEN** Naam, na hilo linanitia wasiwasi!

**114. KABO** Mbona? Wanapendana. Wanapendana kwa dhati ya mioyo yao! Vizuri hivyo. Ni ujana huo!

**Outro:**

Hivyo ndivyo makala ya *Learning by Ear* inavyokamilika hivi leo. Kimekuwa kipindi cha nne cha mfululizo wa "Kukubaliana na Wimbi la Mabadiliko" kuhusu uhamiaji mjini.

Wahusika wetu wanaendelea na harakati zao za kutaka kuanzisha chama cha ushirika. Usikose kipindi kitakachofuata ili ujue kuhusu matayarisho ya mkutano wa kwanza mkuu.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yako, fungua ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe au utuandikie barua-pepe kupitia anwani lbe@dw-world.de.

Kumbuka kusikiliza kipindi kinachofuata!

**END OF EPISODE 4**